

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**  
**مشروع تَعَلُّم الإسلام – أحكام الطهارة - سواحيلي**

**Samo la 8**

**الدرس الثامن**

**DAMU YA HEDHI NA NIFASI.**

Damu ya Hedhi: Ni damu inyotoka katika hali ya afya ya mwanamke, inayotoka katika mfuko wa uzazi wa mwanamke sio kwa ajili ya kujifungua wala maradhi, katika muda maalumu, rangi yake ya kawaida ni nyesusi yenye harufu mbaya.

Damu ya Nifasi: Ni damu inayotoka kutoka kwenye mfuko wa uzazi wa mwanamke kwa sababu ya kujifungua.

Haifai kwa mwenye hedhi au Nifasi kusali au kufunga hali ya kuwa yupo kwenye Hedhi au Nifasi.

من حديث عائشة - رضي الله عنها - قالت: قال رسول الله ﷺ: ((إذا أقبلت الحيضة فدعي الصلاة، وإذا أدبرت فاغسلي عنك الدم وصلي)) [متفق عليه: 331]

Hadithi aliyoipokea mama Aisha mkewe Mtume (saw) anasema. amesema Mtume (saw) : ("Itakapo kujia hedhi basi acha kusali, na itakapo ondoka , basi ioshe damu na usali") ( Ameipokea Bukhari na Muslim:331, 333).

Hata zikidhi swala ambazo hajaziswali kipindi akiwa katika hali ya hedhi, isipokuwa swaumu atazilipa zile siku ambazo hajazifunga, kama vile ambavyo haifai kwa mwenye hedhi kutufu Al-Ka'aba, pia haifai mwanamume kumingilia mwanamke akiwa katika hali ya edhi, lakini inafaa kustarehe naye katika hali ya kuchezeana bila ya kumingilia, pia haifai kwa mwenye hedhi kuushika msahafu.

Atajitwaharisha mwenye hedhi kwa kukatika kwa damu ya hedhi, itamlazimu haraka kuoga ili aweze kujiondoa katika yale ambayo alikuwa amekatazwa kuyafanya.

Atakapo ingia hedhi mwanamke au kuwa na nifasi baada ya kuingia wakati wa swala kabla hajaswali, kauli sahihi ni kwamba atailipa hiyo swala baada ya kutwaharika na hedhi au nifasi.

Atakapo twaharika mwanamke kabla ya kutoka wakati wa swala kwa kiasi cha raka moja hivi, basi itamlazimu kuitekeleza swala hiyo, na inapendezwa azikidhi kwa kukusanya mfano ikiwa ametwaharika kabla ya kuzama jua, basi itamlazimu aswali alasiri na inapendekezwa aikidhi swala ya aduhuri, na ikiwa atatwaharika kabla ya nusu ya usiku basi ataiswali swala ya Ishai na inapendekezwa aikidhi swala ya magharibi.